TANZANIA YOUTH ENVIRONMENTAL NETWORK (TAYEN)

TAYEN
Together We Save the Planet!

JANA ROBEYST TRUST FUND



# MARAFIKI WA TEMBO TANZANIA

*Ushiriki wa Vijana katika Uhifadhi na Ulinzi wa Tembo*

**Evodius Rutta na Pandisha Omary**



Tanzania Youth Environmental Network (TAYEN)
S.L.P 34734, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 (0) 753 062 485, +255 (0) 764 784 257
Barua Pepe: info@tayen.or.tz
Tovuti: www.tayen.or.tz

Kimeandaliwa na TAYEN
ISBN: 978-9976-9906-2-1
@TAYEN, 2017

Haki zote zimehifadhiwa

YALIYOMO


DIBAJI ........................................................................................... 5

SHUKRANI........................................................................................ 7

UTANGULIZI .................................................................................. 8

TEMBO NA TABIA ZAKE ............................................................ 10

FAIDA ZA TEMBO KIUCHUMI NA KIIKOLOJIA ................................ 16

MIGOGORO KATI YA TEMBO NA BINADAMU ................................ 20

UJANGILI WA TEMBO.................................................................. 24

VIJANA NA UHIFADHI WA TEMBO .............................................. 29

MAREJEO ........................................................................................ 31

# DIBAJI

Madhumuni ya Kitabu hiki ni kuwapa fursa vijana waishio maeneo ya karibu na hifadhi za Tanzania kujifunza na kufahamu tabia na maisha ya Tembo; moja kati ya mnyama maarufu anaepatikana kwenye hifadhi za Tanzania. Kitabu kimetolewa kama nyenzo ya kufundishia katika utekelezaji wa shughuli za mradi wa **Marafiki wa Tembo Tanzania** unaotekelezwa kwenye vijiji vya **Kilimani Mashariki** na **Kilimani Magharibi** vilivyopo karibu kabisa ya Pori la Hifadhi la Selous (Selous Game Reserve), Wilaya ya Rufiji, Mkoa wa Pwani**.**

Kitabu kinatolewa wakati ambapo idadi kubwa ya Tembo nchini Tanzania imeteketea kutokana na kukithiri kwa vitendo vya ujangili kwenye maeneo mengi ya hifadhi za Tanzania.Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha takribani asilimia 60 ya Tembo wote walioouwawa kwa ujangili nchini Tanzania, wengi wao walipatikana kwenye Pori la Akiba la Selous. Sababu kuu ya kukithiri kwa vitendo vya ujangili Selous ikiwa ni ukubwa wa eneo la Selous na ushirikishwaji mdogo wa wananchi waishio karibu na Pori la Akiba la Selous kwenye mapambano ya kuzuia vitendo vya Ujangili. Hivyo basi kuna kila sababu ya kuwalenga na kuwashirikisha wananchi waishio maeneo ya karibu na hifadhi katika kupambana na vitendo vya ujangili wa Tembo na wanyama wengine kwenye hifadhi za Tanzania.

Kupitia kitabu hiki vijana hasa waishio maeneno ya karibu na hifadhi watajifunza na kuhamasika kushiriki katika shughuli za Uhifadhi wa Wanyapori na maliasili nyingine. Kitabu kitatumika kama nyenzo ya kuwaandaa vijana kushiriki na kutoa ushirikiano katika kupambana na vitendo vya ujangili wa Tembo kwenye maeneo yote ya hifadhi hapa nchini.

Kwa kuzingatia sera, sheria na miongozo ya serikali ikiwemo Sera ya

Wanyamapori ya mwaka 1998; kitabu hiki kitaongeza ufahamu juu ya Tembo na tabia zake, athari za Ujangili na kuelezea faida ya Tembo kiuchumi, kimazingira (ikolojia) na kisiasa.

## SHUKRANI

TAYEN (Mtandao wa Vijana wa Mazingira), inapenda kutoa shukrani kwa Shirika la **Jana Robeyst Trust Fund** la nchini Uholanzi kwa kufadhili uchapishaji wa kitabu hiki kama nyenzo ya kufundishia Vijana vijiji vya Kilimani Mashariki na Kilimani Magharibi, Wilaya ya Rufiji kuhusu uhifadhi wa mnyama Tembo.

TAYEN inapenda kushukuru serikali za Vijiji vya Kilimani Mashariki na Kilimani Magharibi na uongozi wa Wilaya ya Rufiji, Ofisi ya Mkurugenzi (Idara ya Maliasili) na Uongozi wa Pori la Hifadhi ya Selous kwa kutoa ushirikiano mkubwa wakati wa maandalizi ya kitabu hiki na shughuli nyingine za mradi wa Marafiki wa Tembo Tanzania.

Mwisho shukrani ziende kwa Bodi na wafanyakazi wa wote wa TAYEN kwa kushirki katika maandalizi ya kitabu kwa kutoa mchango wa mawazo na kuboresha uandishi na uaandai wa kitabu hiki toka mwanzo mpaka mwisho.

**TAYEN**
**Dar es Salaam, April 2017**

## UTANGULIZI

Kwa miaka mingi Tanzania imejijengea sifa ya kuwa moja ya nchi iliyobarikiwa kuwa idadi kubwa ya Wanyapori kuliko nchi nyingi barani Afrika na duniani kwa ujumla. Kutokana na sifa hii, Tanzania imekuwa kinara na kujizolea sifa nyingi katika shughuli za Utalii hasa utalii wa maliasili yani Nature Based Tourism. Kupitia utalii Tanzania hutembelewa na wageni mbali mbali toka nchi tofauti ambao huja kama watalii kujionea wanyama mbali mbali wakiwemo Tembo.

Takwimu zinaonyesha shughuli za utalii huchangia asilimia 14 ya pato la Taifa, fedha zipatikanazo kwenye utalii huisaidia serikali kufanya shughuli mbali mbali za maendeleo ya jamii kama ujenzi wa shule, hospitali na miundo mbinu mingine. Lakini kubwa zaidi kupitia shughuli za utalii maelfu ya watanzania wameajiriwa kupitia huduma mbali mbali za kitalii ikiwemo usafiri, malazi (mahoteli) na chakula ndani na nje ya hifadhi za Tanzania.

Historia ya uhifadhi wa wanyama pori nchini Tanzania imeanza mwaka 1891 wakati sheria za kudhibiti uwindaji zilipoanzishwa na serikali ya Kikoloni ya Wajerumani, sheria hii ilidhibiti uvunaji wa wanyama, mbinu za uwindaji na biashara ya wanyama pori.  Pia sheria hii ililenga kuwalinda na kuwatunza wanyama waliokaribia kutoweka (wakiwemo Tembo) kwa kuwekewa mfumo maalumu wa uhifadhi. Mnamo mwaka 1905 ndipo hifadhi ya Pori la Akiba la Selous ilipoanzishwa rasmi, lengo kuu ikiwa ni kulinda na kuwahifadhi wanyama mbali mbali ikiwemo Tembo.

Lakini pia, kutokana na umuhimu wa sekta ya Utalii hasa Wanyapori kama Tembo, mwaka 1998 Tanzania iliweka Sera maalumu ya Usimamizi wa Wanyamapori, hii inaendana na kutambua na kuyalinda maeneo waishio wanyama hao kama

Hifadhi za Taifa (National Park). Kupitia sera hiyo, serikali inaweza kuyasimamia kwa ukaribu maeneo yote ya hifadhi na kuwa na utaratibu mzuri wa kuwalinda wanyama wote waishio kwenye maeneo ya hifadhi. Mfano kupitia sera na sheria za Utalii na Wanyapori serikali ilianzisha Mamlaka ya Hifadhi za Taifa yani TANAPA kama taasisi maalumu chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kusimamia uhifadhi, ulinzi na usimamizi wa wanyapori.

Pamoja na juhudi zote za serikali kuwalinda na kuwahifadhi wanyapori nchini, hivi karibuni vitendo vya ujangili wa mnyama Tembo vimekuwa vikiongezeka kwa kasi sana kwenye maeneo ya hifadhi. Moja kati ya hifadhi zilizoathirika kwa kiasi kikubwa kwa vitendo vya Ujangili ni Pori la Akiba la Selous (Selous Game Reserve). Takwimu za Wizara ya Maliasili zinaonyesha katika kipindi cha miaka 10, Selous imepoteza zaidi ya asilimia 60 ya Tembo wake, wakati kulingana na takwimu za shirika la kimataifa la Habari la Aljazeera zinaonyesha kwa mwaka 2006 pekee, Tanzania ilipoteza zaidi ya Tembo wake 10,000. Wengi wa Tembo hawa walikuwa wakipatikana kwenye Pori la Akiba la Selous.

Kutokana na ukubwa wa tatizo la Ujangili wa Tembo Tanzania na umuhimu wa kushirikisha wananchi hasa Vijana katika kupambana na ujangili. Maelezo ya kitabu hiki yanalenga kumwelimisha kijana kuhusu tabia na maisha ya Tembo, athari za vitendo vya ujangili na kutoa hamasa kwa Vijana kulinda, kuhifadhi na kutoa ushirikiano katika kupambana na vitendo vya Ujangili nchini. Kitabu hichi kimegawanywa katika Mada Tano: Tembo na Tabia zake, Umuhimu wa Tembo (Kiuchumi na Kiekolojia), Migogoro kati ya Tembo na Binadamu, Ujangili wa Tembo na Athari zake na Vijana na Uhifadhi wa Tembo.

### SOMO LA KWANZA

## TEMBO NA TABIA ZAKE

### 1. Je Tembo ni Mnyama wa aina Gani?

### 1.1. Maumbile ya Tembo


Tembo ni mnyama mkubwa miongoni mwa jamii ya wanyama wanaozaa na kula majani. Tembo huishi kwa zaidi ya miaka 60. Kimaumbile Tembo huwa na urefu wastani kati ya mita 2.5 mpaka 4 kwa Tembo mkubwa wakati mita 1 au 1.5 kwa Tembo mtoto. Kwa upande wa uzito, uzito wa Tembo unatofautiana kulingana na jinsia na umri wa Tembo, Tembo jike huwa na uzito wa kilo kati ya 2750 hadi 3250, wakati Tembo dume huwa na uzito usio pungua kilo 5000 hadi 6000, wakati Tembo mtoto hua na kilo zisizopungua 91 hadi 100. Kuna aina kuu mbili za Tembo, ambazo hupatikana barani Afrika na Asia.

Tembo kama wanyama wengine wazaao hubeba mimba ambayo huchukua takribani miaka miwili mpaka kuzaa kwake. Mara nyingi tembo huzaa mtoto mmoja tu na ni mara chache sana hutokea kuzaa mapacha. Kimaumbile Tembo wanaopatikana Afrika (African Elephants) ndio wakubwa kuliko wote Duniani.

### 1.2. Masikio na Meno ya Tembo

Kwa upande wa wanyama wanaokula majani, Tembo ni mnyama mwenye masikio makubwa sana, ukubwa wa masikio yake humsaidia katika kupunguza joto la mwili wake kwa njia ya kujipepea hasa wakati wa joto kali. Kwa mbele, Tembo huwa na Mkonga (Pua) ndefu ambao hutumia kupumua na kuvuta hewa, kuchukulia chakula, kutoa ishara ya hatari au furaha kwa wenzake. Mkonga pia hutumika kama mkono kuvunja au kuchukua vitu mbali mbalia chini au juu ya

miti au ardhini. Pia Tembo huwa na Meno mawili yaliyotokeza kwa mbele yenye rangi nyeupe, meno haya au kwa jina lingine Ndovu hutumika kwa kazi mbali mbali ikiwemo kuchimba mizizi ardhini, kukata miti na kujilinda na maadui wakati wa hatari. Meno ya Tembo ni tofauti na meno ya wanyama wengine, kwani meno yake hubadilika mara tatu wakati wa uhai wake.





**Kielelezo 1: Meno na Masikio ya Tembo katika picha**

## 1.3. Mkia wa Tembo

Kama ilivyo kwa wanyama wengine, Tembo huwa na mkia ambao huutumia kufukuzia wadudu wasumbufu ikiwemo mbung'o, ndege na wengine. Ukubwa wa mwili wake unaendana na ukubwa wa Miguu yake, pamoja na kuwa na miguu na mwili mkubwa Tembo huweza kukimbia zaidi ya kilomita 30 kwa saa.

## 1.4. Makazi na Malazi ya Tembo

Tembo huishi porini kwenye maeneo yenye joto la wastani, kwenye vichaka na majani, yasio na miti mikubwa. Kwa kuwa maumbile yake ni makubwa sana,

Tembo huitaji kuishi eneo lenye ardhi kubwa, maji na chakula cha kutosha. Ngozi ya Tembo humfanya kujilinda na wadudu hatarishi kama Nyuki na Mbu ambao huweza kushambulia ngozi yake. Kwa sababu hiyo, Tembo huweka makazi yake au kuishi mbali na wadudu hao. Tembo pia huishi kwenye maeneo yanayopatikana maji mengi, hii inatokana na mahitaji yake ya maji ambayo yanaendana na maumbile yake, Tembo huitaji maji mengi kunywa na kupoza ngozi yake wakati wote.

## 1.5. Chakula cha Tembo

Tembo hula nyasi, magome ya miti, matunda, mizizi na hata majani ya miti aina yote, ulaji wa majani ya aina ya miti tofauti humfanya Tembo kupunguza ushindani wakujipatia chakula na wanyama wengine kama Twiga, jamii ya Nyati na Nyumbu ambao pia hula vyakula hivyo. Kwa kuwa maumbile makubwa Tembo mkubwa hula zaidi ya kilo 139 kwa siku, wakati Tembo mdogo hula chini ya kilo 100. Kwa ulaji huu, Tembo husaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza vichaka na kusambaa ovyo kwa majani maeneo ya hifadhi.



**Kielelezo 2: Tembo wakila majani na maboga**

## 1.6. Tabia na Maisha ya Tembo

### 1.6.1. Ubongo na uwezo wa Akili za Tembo

Wataalmu wa wanyamapori hasa mnyama Tembo wanakadiria Ubongo wa Tembo kuwa na wastani wa kilo 4.8. Kwa ukubwa wa ubongo huu wanasayansi wa wanyama humuweka Tembo kuwa mmoja wa wanyama wenye akili nyingi sana. Kulingana na tafiti mbali mbali, ukubwa wa Ubongo wa Tembo humfanya Tembo kuwa na kumbukumbu ya mda mrefu sana, kuwa na hisia kali ikiwemo hisia za furaha na huzuni. Tabia hizi zimefanya Tembo afananishwe na uwezo wa binadamu kukumbuka na kuwa na hisia kali pale matukio mbali mbali yanapo mtokea.

Mfano, katika hali ya kushangaza Tembo kumtambua Mzazi wake hata pale anapopoteana nae kwa mda mrefu. Pia, Tembo huwa na hisia za huzuni kali pale mwenzake au mwenzao kufa, kama wanyama hufanya mazishi kwa kumfunika na matawi ya miti na kusimama kwa dakika kadhaa kwa utulivu na kisha kufukia mwili wake kwa miti. Pia Tembo huweza kukumbuka njia aliyopita hata baada ya miaka 15 kupita, kumbukumbu ya njia hii hubaki kwa mda mrefu kwenye akili yake. Kutokana na uwezo mkubwa wa akili ya Tembo, barani Asia Tembo baadhi ya nchi humtumia  Tembo kutoa burudani kwa kufanya michezo kama mpira, kubeba au kusafirisha mizigo, na Tembo huweza kumtambia mhusika wa mzigo kwa sura zao na sauti.




**Kielelezo 3: Tembo akiwa na huzuni baada ya kumpoteza mwanae**

### 1.6.2. Malezi ya Tembo

Tembo huishi katika makundi kama familia au ukoo mmoja, makundi haya yamegawanyika kulingana umri na jinsia. Mara nyingi kundi kubwa au ukoo huwa na Tembo Jike na watoto wake, kundi hili huongozwa na mwanamke mkubwa kiumri ambae huwaongoza kama kiongozi. Na kama ikitokea kingozi huyu amefariki, anaefatia kiumri huchukua hayo majukumu. Kundi la pili la Tembo huusisha vijana wa kiume ambao huachana na Mama zao pale tu wanapofikisha miaka 15 hadi 17. Baadae kundi hili la Tembo vijana huungana na kundi la Tembo wakiume wakubwa na kuishi pamoja.



**Kielelezo 4: Kundi ka Tembo likiambatana kama Familia**

## SOMO LA PILI

## FAIDA ZA TEMBO KIUCHUMI NA KIEKOLOJIA

### 2.1. Je Tembo ana faida yoyote Kwangu?

Tanzania ni moja ya nchi zilizobarikiwa kuwa na maliasili nyingi hasa Wanyapori ikiwemo Tembo na wanyama wengine maarufu. Kwa miaka mingi Tanzania imejijengea sifa barani Afrika na dunia nzima kuwa moja ya nchi yenye idadi kubwa ya wanyamapori hasa Tembo. Kulingana na takwimu za hv karibuni Tanzania inakadiriwa kuwa na wastani wa Tembo kati ya 100,000 mpaka 200,000, nchi nyingine barani Afrika zenye idadi kubwa ya Tembo ni Kenya, Gabon na Congo DRC.

Kwa upande wa Tanzania idadi kubwa ya Tembo hao, takribani asilimia 60 ya Tembo wote wa Tanzania wanapatikana kwenye Pori la Akiba la Selous (Selous Game Reserve) na wengine wengi kupatikana kwenye hifadhi ya Mikumi na hifadhi nyingine nchini. Kufuatia uwepo wa Tembo wengi na wanyama wengine, na ukubwa wa Pori la Akiba la Selous, Shilika la Umoja wa Mataifa Elimu na Utamaduni (UNESCO) liliipa sifa Selous kuwa moja ya maeneo adimu ya hifadhi duniani maarufu kama World Heritage Site. Sifa hii imeiletea sifa nyingi Selous na hivyo kuifanya kuwa kivutio kikubwa cha watalii ndani na nje ya nchi ambao huja kuangalia Tembo na wanyama wengine.

### 1.2. **Faida za Tembo**

#### 1.2.1. **Kiuchumi**

Uwepo wa Tembo kwenye hifadhi zetu huvutia watalii wengi toka ndani na nje ya Tanzania ambao kuangalia Tembo na wanyama wengine maarufu wapatikano

kwenye hifadhi za Tanzania. Uwepo na ujio wa watalii huchochea shughuli za utalii hasa huduma za malazi, usafiri, chakula na nyinginezo kwa watalii. Hii hufanya watanzania wengi hupata ajira na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa uchumi wa Tanzania hasa pato la taifa kupitia makusanyo ya kodi mbali mbali. Kulingana na takwimu za serikali shughuli za utalii huchangia kwa asilimi 14 ya pato la Taifa yani GDP. Kodi ipatikanayo kwenye utalii hutumika kuboresha huduma za jamii ikiwemo Shule, Barabara, Hospitali na miundo mbinu mingine.



**Kielezo 5: Watalii wakifurahia mnyama Tembo kwenye hifadhi**

### 1.2.2. **Kimazingira (Kiekolojia)**

Tembo ni myama mwenye umuhimu sana katika ekolojia na mifumo ya utegemezi ya chakula ndani ya hifadhi. Hii hutokana na uwezo wa Tembo kula takribani kilo 139 kwa siku , kitendo hiki hupelekea kupungua kwa mrundikano wa vichaka na kutoa uwazi kwa mimea mingine hasa majani kuota na kurahisisha mfumo wa chakula kwa viumbe vingine. Lakini pia hii husaidia katika mtawanyiko wa aina tofauti tofauti ya mimea ndani ya hifadhi. Kinyesi cha Tembo ambacho huwa ni

kikubwa na hivyo huongeza rutiba kwenye udongo na hivyo kuchochea ukuaji wa majani na miti kwenye maeneo mengi ya hifadhini na hivyo kuboresha ustawi wa mazingira.



**Kielelezo 6: Tembo akila matawi ya mti**

Kwa kuwa Tembo hunywa na kutumia maji mengi, hii humpa uwezo wa kujua sehemu mbali mbali zenye maji ardhini na kuchimba mashimo ya maji ama vijisima kwa kutumia Mkonga wake hasa wakati wa kiangazi. Hii huwawezesha wanyama wengine kujipati maji kupitia kwa Tembo. Kwa ufupi uwepo wa Tembo husababisha ukuaji na ustahimili wa wanyama wengine wanaotegemea mienendo ya maisha ya Tembo. Hivyo basi kuhama au kutokuwepo kwa Tembo huweza pia kuharibu mfumo mzima wa chakula na uhai wa wanyama wengine.



**Kielelezo 7: Kundi la Tembo likiwa na wanyama wengine wakinywa maji**

## SOMO LA TATU

# MIGOGORO KATI YA TEMBO NA BINADAMU

### 3.1. Nini Husababisha Wanadamu kugombana na Tembo.

Katika kulinda na kuhifdhi mipaka yake, Tembo hutumia akili zake kuhifadhi na kulinda mipaka yake kimazingira ili kujihakikishia usalama. Na kwa kuwa Tembo huitaji ardhi kubwa kwa chakula na malazi, hali hii husababisha kuhama hama hapa na pale katika kutafuta mahala salama anakoweza kupata chakula na malazi kwa urahisi. Hali hii ya kuhama hama, husababisha Tembo kuwa na mgogoro na binadamu hasa waishio maeneo ya karibu na hifadhi.

### 3.2. Chanzo na Athari za Migogoro.

### 3.2.1. Mahitaji ya Ardhi kati ya Binadamu na Tembo

Kwa kuwa Tembo ni myama mkubwa, hivyo huitaji ardhi kubwa kwa chakula na malazi, hali hii husababisha Tembo kutembea umbali mrefu kwenye eneo kubwa la ardhi ili kuweza kujipatia chakula na maji kulingana na msimu na eneo husika. Ongezeko la watu kwenye maeneo mengi hasa vijijini limechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi na maji kwa matumizi ya kilimo, makazi na matumizi mengine ya binadamu. Hali hii imemechochea kwa kiasi kikubwa kwa mwanadamu hasa waishio maeneo karibu ya hifadhi kuanzisha mashamba na makazi hata ndani ya maeneo ya hifadhi.

Kutokana na hilo, kwa muda mrefu kumekuwa na muingiliano mkubwa kati ya Tembo na wanadamu, na hivyo kuleta migogoro kati ya Tembo na wanadamu wakigombea ardhi. Mfano hai, ni pale Tembo wanapovamia mashamba ya wanadamu na kula mazao. Matukio kama haya yamekuwa menggi sana maeneo ya karibu na hifadhi na mara nyingine kusababisha Tembo kuuwawa au binadamu

kushambuliwa na Tembo akiwa shambani.



**Kielelezo 8: Tembo wakiwa wamevamia maeneo ya binadamu**

### 3.1.2. Vitendo vya Ujangili

Ujangili ni shughuli zozote za uwindaji au uvunaji wa maliasili ikiwemo misitu au wanyamapori kinyume na sheria za nchi. Vitendo vya ujangili ni moja kati ya chanzo kikubwa katika kutokea kwa migogoro kati ya binadamu na Tembo. Katika kipindi cha hivi karibu binadamu wamekuwa wakijihusisha sana na kuua Tembo kama njia ya kujipatia kipato kwa kuuza meno yake.

Vitendo hivi vimechangia sana kuwepo kwa chuki kati ya Tembo na binadamu. Hali imesababisha Tembo kumwona binadamu kama adui yake namba moja na hivyo kufanya uharibifu mkubwa sana kwenye maeneo ya makazi au mashamba ya binadamu kama njia ya kulipiza kisasi.

Ikumbukwe Tembo huwa kumbukumbu kubwa sana ya matukio, hali hii humfanya kukumbuka matukio ya kijangili yanayotokea kwa Tembo wenzake na hivyo kumfanya kuwa na chuki na binadamu na hata kupanga kulipiza visasi kwa binadamu. Kulingana na tafiti zilizofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa nchini Tanzania (TANAPA), tafiti zinaonesha kuwa maeneo mengi yaliyokithiri kwa vitendo vya ujangili, migogoro ya Tembo na Binadamu haiepukiki.



**Kielelezo 9: Mauaji ya Tembo kwa njia ya Ujangili**

## 3.3. Jinsi ya kutatua migogoro kati ya Tembo na Binadamu.

Kuna njia mbali mbali za kutatua migogoro kati ya Tembo na binadamu, lakini kabla la kuzijua njia hizo ni vema tukatambua kuwa binadamu ndo chanzo kikuu cha migogoro kati ya Tembo na yeye. Hii husababishwa na binadamu kumfata au kuingilia makazi au ardhi ya Tembo kwa kuanzisha makazi au mashamba maeneo waishio Tembo. Zifuatazo ni baadhi ya njia za kutatua au kuepuka migogoro kati ya Tembo na wanadamu

Moja, ni vizuri wanadamu wakaheshimu mipaka na maeneo yote hifadhi kwa kutoanzisha makazi au mashamba au kupeleka mifugo kwenye maeneo waishio Tembo. Katika kufanikisha hili, viongozi wa Serikali ya kijiji hawana budi kushirikiana na Serikali Kuu kusimamia na kuwakumbusha wananchi mipaka ya maeneo ya hifadhi na mwisho wa maeneo yao ya kufanya shughuli za kilimo, makazi au ufugaji wa mifugo. Ni vema pia maeneo yote pamoja na njia ambazi Tembo hupita mara kwa mara yakawekwa alama maalumu zitakazotambulika kirahisi na wanadamu kuzuia wanadamu kuingilia makazi na njia za Tembo.

Pili, ni kinyume na sheria na kosa la jinai kwa wanadamu kushiriki moja kwa moja au kushirikiana na majangili kwenye vitendo vya Ujangili. Ni vema basi wananchi wakashirikiana na vyombo vya dola katika kupambana na Ujangili kwa kutoa taarifa kwa watu wote wanaojihusisha na shughuli za Ujangili. Kutokuwepo kwa vitendo vya ujangili huleta amani kati ya wanadamu na Tembo.

Tatu, ufugaji wa Nyuki ni moja ya njia maarufu itumikayo sehemu nyingi duniani katika kuondoa migogoro kati ya Tembo na wanadamu. Hapo nyuma tumejifunza baadhi ya wadudu ambao si rafiki wa Tembo, nyuki ni mojawapo ya wadudu hao, Tembo huogopa sana nyuki kwa kuhofia kung'atwa ngozi yake, na kwa sababu hiyo Tembo hukaaa mbali sana na maeneo waishio Nyuki. Na kwa kuwa nyuki wana faida nyingine nyingi kama upatikanaji wa asali, basi ni vema wanadamu wakafuga nyuki kwenye maeneo ya mashamba na makazi ili kuzuia Tembo kuingia kwenye maeno hayo.

## SOMO LA NNE

## UJANGILI WA TEMBO

### 4.1. Ujangili ni Nini?

Ujangili ni shughuli zozote za uwindaji au uvunaji wa rasilimali ikiwemo maliasili za mistu au wanyamapori kinyume na sheria za nchi. Ujangili wa Tembo huhusisha uuwaji wa Tembo kwa lengo la kujipatia kipato kwa kuuza Meno yake maarufu kama Ndovu za Tembo (Ivory). Vitendo vya Ujangili vinachangiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na kuongezeka kwa mahitaji makubwa ya Meno ya Tembo kwenye masoko ya bara la Asia hasa nchi za China na Vietnam. Katika nchi hizi Meno ya Tembo au Ndovu hutumika kutengenezea urembo kwenye vitu vya thamani kama vidani, viti, na urembo mwingine.

Kihistoria, vitendo vya Ujangili vilianza zamani toka enzi za uvamizi wa waarabu toka Mashariki ya Kati wakati wa kipindi cha ukoloni ambapo Waarabu walitumia meno au ndovu za Tembo kutengenezea vitu mbali mbali hasa urembo wa nyumbani. Kwa Tanzania vitendo vya ujangili vimeathiri sana ukuaji na ustawi wa Tembo.

Kulingana na takwimu za Shirika la Kimataifa la Uhifadhi la WWF, katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, Tanzania imepoteza takribani asilimia 60 ya Tembo wake kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya Ujangili kwenye maeneo mengi ya hifadhi za Taifa ikiwemo Pori la Akiba la Selous. Hali hii imechangia na kuhatarisha kupotea kabisa kwa uwepo wa mnyama Tembo nchini.



**Kielelezo 10: Jangili akivuna Meno ya Tembo**

## 4.2 Je nini athari za Ujangili?

### 4.2.1. Athari za Ujangili Kiuchumi

Kama tulivyojifunza hapo nyuma, uwepo wa mnyama Tembo huvutia wageni yani watalii wengi ndani na nje ya Tanzania na hivyo kulileteа Taifa letu pesa nyingi kupitia mapato yanayo kusanywa kwenye shughuli za utalii. Hivyo basi vitendo vya Ujangili huhatarisha kutokuwepo kwa mnyama Tembo ambae ndio kivutio kikubwa cha watalii. Hali hii husababisha kupotea kwa mapato mengi

kupitia kwenye shughuli za utalii, kwani matukio ya Ujangili pia huzua hofu kwenye maeneo ya hifadhi na hivyo kupungua kwa kasi sana uwepo wa watalii kwenye maeneo ya hifadhi ambao huofia usalama wao. Hii pia huathiri mfumo mzima wa utalii kwa watalii kutopenda kutembelea maeneo ya hifadhi hata kama Tembo wapo maana huofia usalama wao.

### 4.2.2. Athari za Ujangili Kijamii na Kisiasa

Kuwepo kwa vitendo vya Ujangili nchini Tanzania huiondolea sifa Tanzania kama moja ya nchi barani Afrika yenye idadi kubwa wa Tembo. Kisiasa sifa hii huweza kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kimataifa na hivyo kuvutia watalii wengi nje ya Tanzania ambao huja kutembelea hifadhi za Tanzania. Shughuli za Ujangili huleta hofu kwa wananchi hasa waishio maeneo ya karibu na hifadhi ambao huishi kwa hofu, hali hii inasababishwa kwa kuwa vitendo vya ujangili huusisha matumizi ya silaha kubwa za moto katika kutekeleza mauaji ya Tembo. Matumizi ya silaha hizi huweza kuleta madhara ya usalama, mana silaha zitumikazo kwenye ujangili zinaweza kutumiwa kwenye matukio mengine ya hatari kama ujambazi na utekaji wa wananchi.

### 4.2.3. Athari za Ujangili Kimazingira

Kwa kuwa Tembo huzaa mara moja tu na kuishi zaidi ya miaka 60, na mara nyingi Ujangili huusisha mauaji ya Tembo wakubwa ambao ni wazazi na walezi wa Tembo wadogo, hali husababisha kupungua kwa kasi ya kuzaliana kwa Tembo na hivyo kuhatarisha kabisa uwepo wa Tembo duniani. Lakini pia, kama tulivyojifunza hapo nyuma, uwepo wa Tembo husaidia ukuaji na ustawi wa wanyama wengie wanaokula majani na miti kama Tembo. Hivyo basi, mauaji ya Tembo huvuruga mfumo mzima wa ukuaji na ustawi wa wanyama wengine

ambao kwa namna moja au nyingine hutegemea maisha ya Tembo.

### 4.3 Je njia zipi hutumika kupambana na Ujangili?

Kulingana na ukubwa wa tatizo la ujangili zipo njia nyingi tofauti zinazotumika katika kupambana na tatizo hili kubwa. Zifuatazo ni baadhi ya njia zinazotumika kupambana na Ujangili nchini:

- **Kuongeza Ulinzi wa Tembo kwa kufanya doria za mara kwa mara kwenye maeneo waishio ama kupita Tembo**. Njia hii huusisha maafisa wa Wanyapori kwenye hifadhi kufanya Doria au Patrol kwa njia za Miguu na Magari, na saa nyingine hata vyombo vya anga kama Helikopta kwenye maeneo yote ya hifadhi hasa maeneo ya katikati ya hifadhi wanapoishi Tembo kwa uwingi.

- **Kuwashirikisha moja kwa moja wananchi wanaoishi maeneo ya hifadhi katika mikutano na doria kama njia ya "Ujirani Mwema":** Lengo la njia hii kuwapa fursa wananchi waishio karibu kuweza kushirikiana na Maafisa au uongozi wa hifadhi kutoa taarifa pale wanapohisi kuna mwananchi anashiriki au anashirikiana na majangili katika kutekeleza vitendo vya Ujangili.

- **Matumizi ya Ndege zisizo na Rubani maarufu kama "Drone**": Njia hii ni ya tekinolojia ya kisasa iliyoletwa hapa nchini miaka ya hivi karibuni. Njia hii huhusisha matumizi ya vindege vidogo maarufu kama Drone ambavyo huwa na kamera. Ndege hizi zisizo ndogo zisizo na rubani huwa na uwezo wa kuruka juu umbali wa hata futi 30 na kwenda zaidi ya kilimota 20 kupiga kupicha za eneo la hifadhi na kuzituma picha hizo kwenye ofisi za hifadhi. Mara nyingi njia hii huusisha kutuma ndege hizi kwenda kupiga picha maeneo waliopo Tembo ili kuonyesha hali ya Tembo eneo walipo.

- **Kushirkiana na jumuiya Kimataifa katika kupambana na Ujangili**. Kwa kuwa tatizo la ujangili sio la Tanzania pekee bali ni tatizo la Dunia nzima. Serikali ya Tanzania ikishirikiana na jumuiya ya kimtaifa kupitia Wizara ya Maliasili na Utaliii inashikirikiana na serikali mbalimbali hasa nchi za Asia ikiwemo China katika kupinga na kuzuia uuzwaji au ununuzi wa biadhaa zote zinazozalishwa kwa kutumia Meno au Ndovu za Tembo. Hali imepunguza kwa kiasi kikubwa mahitaji ya pembe au meno ya Tembo katika masoko ya bara la Asia ambayo ndo kichochocheo kikubwa cha Ujangili.



**Kielelezo 11: Aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mh. Lazaro Nyalandu akisaini mkataba wa kimataifa katika kupambana na Ujangili**

## SOMO LA TANO

## VIJANA NA UHIFADHI WA TEMBO

### 5.1. Nini Mchango wa Vijana katika Uhifadhi wa Tembo?

Takwimu za sensa ya Taifa ya mwaka 2012 zinaonyesha Tanzania ina takribani watu milioni 46, asilimia 68 ya idadi hii ni Vijana chini ya umri wa miaka 15. Wengi wao wakiishi vijijini hasa karibu na maeneo ya hifadhi za Taifa na maliasili nyingine. Hivyo basi, vijana ambao ndo kundi kubwa la wananchi wote wa Tanzania, hawana budi kushiriki katika shughuli za uhifadhi wa Tembo na maliasili nyingine zipatikanazo Tanzania. Kwa ufupi uwepo wa Tembo leo na kesho, unawahakikishia ustawi wa maisha bora Vijana na kizazi kijacho kupitia faida mbali mbali za Tembo na maliasili nyingine kama tulivyojifunza hapo nyuma.

### 5.2. Je vipi naweza kushiriki kuhifadhi na kumlinda Tembo

Tembo ni mmoja ya wanyama maarufu kwenye mbuga zetu, kwa sifa hii, vijana hatuna budi kushiriki na kushirikiana na serikali katika kuwatunza, kuwalinda na kuwahifadhi. Zifuatazo ni njia mbali mbali ambazo kama Kijana unaweza kushiriki na kushirikiana na serikali katika uhifadhi na ulinzi wa Tembo

- Baada ya kusoma kitabu hiki, shiriki na wenzako kwa kutoa Elimu kwa jamii yako kuhusu uhifadhi wa Tembo na faida zake. Unaweza kutoa elimu ukiwa shuleni, nyumbani, mtaani na hata kwenye maeneo ya ibada kama Kanisani na Msikitini.

- Shirikiana na wenzako kuandaa shughuli za uhifadhi wa mazingira ikiwemo

kupanda miti ya kivuli na ya matunda kwenye maeneo ya kijiji na shuleni kwako. Ikumbukwe kuwa ustawi wa mazingira ni ustawi na ukuaji bora wa Tembo.

- Toa taarifa kwa serikali ya Kijiji au vyombo vya Dola pale unapohisi au kusikia mwananchi yoyote ndani au nje ya Kijiji chako anajishugulisha au kushirikiana na majangili katika kutekeleza vitendo vya Ujangili.

- Shiriki kwenye mikutano ya Kijiji chako na omba kujulishwa kuhusu maendeleo ya shughuli za uhifadhi wa Mazingira na wanyamapori kwenye kijiji chako.

- Shiriki na wenzako kuandaa safari ya masomo kutemelea hifadhi za Taifa kwenda kuangalia na kujifunza zaidi kuhusu mnyama Tembo na wanyama wengine wengi wapatikanoa kwenye hifadhi nyingi Tanzania.

## MAREJEO


1. Lauren P & J.J. Mwanang`ombe (2011). Threatened Animals Of East Africa. Jamama Printers Limited, Dar es Salaam, Tanzania.
2. Wildlife Trade Monitoring Network (TRAFFIC). 2012. Illegal hunting and trade of wildlife in savannaAfrica may cause conservation crisis. ScienceDaily, 12 October 2012.
3. WWF, 2016. Saving Selous, African Icon under Threat, WWF Analysis by Dalberg, June 2016.
4. Worldwide Fund for Nature (WWF) 2015. Human-Elephant Conflict.
5. http://www.aljazeera.com/news/asiapacific/2014/11/report-africa-ivory-smuggled-china-visit 201411163317314744.html
6. www.ifaw.org/education
7. www.tnrf.org

Tanzania Youth Environmental Network (TAYEN)
S.L.P 34734, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 (0) 753 062 485, +255 (0) 712 255 843
Barua Pepe: info@tayen.or.tz
Tovuti: www.tayen.or.tz

# Tanzania Youth Environmental Network (TAYEN)

# Marafiki wa Tembo Initiative

JANA ROBEYST TRUST FUND


## Engaging Youth in combating Poaching in Tanzania

## Project Area

Selous Game Reserve is Africa's largest protected area and UNESCO World Heritage Site found in southern Tanzania. It is a home to one of the greatest concentrations of African elephants on the continent, but rampant ivory poaching has seen the population reduced by 90 per cent in less than 40 years. According to World Wide Fund (WWF) the loss of Selous' elephants would have a negative effect on Tanzania's nature based economy, putting the livelihoods of 1.2 million people at risk. Travel and tourism in Selous generate US$6 million annually.


Recognizing this, the project will be implemented in **Kilimani Mashariki** and **Kilimani Magharibi** villages, the two villages are adjacent to Selous Game Reserve in Rufiji District. The project will engage over 50 village youths through wildlife education and educational visits to SELOUS Game Reserve. This will have a long term impact to youth now and in the future.











## The Problem

In 2006, Tanzania lost over 10,000 African Elephants due to illegal poaching fueled by increased demand for ivory in Asian markets of China and Vietnam. To address this, the government of Tanzania in collaboration with international conservation NGOs have initiated various programs to control and stop poaching in the country. However, most of these programs have been focusing on strengthening law enforcement and improving technologies to track movements of elephants. Little has been done to engage village youths living adjacent to protected areas as a potential solution to illegal poaching.

## Why Youth?

In 2014, 45 percent of Tanzania's population were youth under 15; by 2030 the population is projected to be 79.4 million. Today's youths are tomorrows community leaders and policy makers, if informed and imparted with conservation knowledge, young people especially those adjacent to protected areas (**National Parks**, **Nature Reserves, Game Reserve** etc) provide a long term solution for solving local conservation problems.


**Project Goal:** Impart conservation knowledge and empower village youths to protect African Elephants.

## Project Outputs

- Increased awareness among youth on wildlife conservation and poaching.
- 50 youths engaged in wildlife conservation training in and outside their villages.
- "Marafiki wa Tembo" youth groups established in project villages

## Project Timeline

### Flowchart of Activities




## References


- http://www.aljazeera.com/news/asiapacific/2014/11/report-africa-ivory-smuggled-china-visit 2014116163317314744.html
- Population Reference Bureau, "2015 World Population Data Sheet', 2015.
- WWF, 2016. Saving Selous, African Icon Under Threat, WWF Analysis by Dalberg, June 2016.


TAYEN
Together We Save the Planet!


**Project Coordinator**
Evodius Waziri Rutta
Email: erutta@tayen.or.tz
Phone: +255 (0)713-527 551
Website: www.tayen.or.tz